

SEKTA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA

1.0 UTANGULIZI

Asilimia 87 ya wakazi wa wilaya ya Chunya wanategemea kilimo na kilimo ndiyo huchangia kwa kiwango kikubwa sana uchumi wa Wilaya.

Wilaya inakadiriwa kuwa najumla ya eneo lenye ukubwa wa hekta 1,315,000 ambapo eneo linalofaa kwa kilimo linakadiriwa kuwa ni hekta 1,035,400 na jumla ya hekta 79,072 ndizo zilizotumika kwa kilimo cha mazao ya chakula, biashara na bustani(mboga na matunda) katika msimu wa kilimo 2016/2017.

Hata hivyo eneo linalolimwa hubadilika kila msimu kulingana na malengo ya wakulima na mwelekeo wa hali ya hewa

Mazao ya chakula yanayolimwa ni Mahindi, Viazi vitamu, Maharage, Ulezi, Mtama, Mpunga, Muhogo na Kunde. Mazao ya biashara ni Tumbaku, Karanga, Alizeti, Ufuta na Choroko.

2.0 HALI YA HEWA

Wilaya ina wastani wa joto kati ya nyuzi za sentigredi 21 na 23. Wilaya hii hupata aina moja ya mvua (Unimodal rainfall pattern) yenye wastani kati ya milimita 500 na 1000 kwa mwaka. Msimu wa mvua huanzia mwishoni mwa mwezi Oktoba hadi Aprili na kipindi chenye mvua nyingi ni kati ya mwezi Januari na Machi.

3.0 KANDA ZA MAZAO (AGRO – ECOLOGICAL ZONES)

Wilaya ina kanda kuu 2 nazo ni ukanda wa madini na ukanda wa miombo.

3.1 Ukanda wa madini : Ukanda huu unajumuisha maeneo yote ya Tarafa ya Kiwanja yenye kata 11, vijiji 19 na mitaa 35. Mazao yanayolimwa ni Mahindi, Maharage, Mtama, Karanga, Viazi vitamu, Ulezi, Mihogo na Alizeti

3.2 Ukanda wa miombo : Ukanda huu unajumuisha maeneo yote ya Tarafa ya Kipembawe yenye kata 9 na vijiji 24. Mazao yanayolimwa ni Mahindi, Tumbaku, Alizeti, Kunde, Choroko, Maharage, Mihogo, Viazi vitamu, Ulezi na Karanga

4.0 MALENGO YA IDARA

4.1 Lengo Kuu

Kuboresha huduma za kilimo ili kuchangia uhakika na usalama wa chakula na kupunguza umaskini wa kipato kwa wakulima.

4.2 Malengo Mahususi

- i. Kuongeza tija ya uzalishaji kwa zao la mahindi kutoka 2.0 tani kwa hekta ya mwaka 2015 hadi 4.0 tani kwa hekta ifikapo 2025.
- ii. Kuongeza tija ya uzalishaji kwa zao la mtama kutoka 1.6 tani kwa hekta ya mwaka 2015 hadi 3.5 tani kwa hekta ifikapo 2025.
- iii. Kuongeza tija ya uzalishaji kwa zao la alizeti kutoka 1.8 tani kwa hekta ya mwaka 2015 hadi 3.0 tani kwa hekta ifikapo 2025.
- iv. Kuongeza eneo linalolimwa zao la alizeti kwa kaya kutoka hekta 1.2 ya mwaka 2015 hadi hekta 2.0 ifikapo 2025
- v. Kuongeza idadi ya vyama vya ushirika wa wakulima vilivyo sajiriwa kutoka 39 ya mwaka 2015 hadi 50 ifikapo 2025.
- vi. Kuongeza na kuboresha miundo mbinu ya kilimo ifikapo mwaka 2025

5.0 HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA NJIA ZINAZOTUMIKA

5.1 Huduma zinazotolewa

- Kusimamia maandalizi na utekelezaji wa malengo ya uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na bustani (Mboga na Matunda).
- Kuelimisha wakulima mbinu bora za kilimo cha mazao ya chakula, biashara na bustani. Elimu itolewayo ni kanuni za kilimo bora, matumizi sahihi ya zana bora katika kuboresha kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji, mbegu bora na matumizi sahihi ya mbolea.
- Kuelimisha wakulima juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu na njia sahihi za udhibiti wa magonjwa ya mazao na wanyama waharibifu.
- Kuwatembelea wakulima, kuona changamoto wanazokutana nazo na kutoa ushauri wa jinsi ya kutatua changamoto hizo.
- Kuelimisha wakulima juu ya utayarishaji, usindikaji na hifadhi bora ya mazao baada ya mavuno pamoja na ukadriaji wa mahitaji ya chakula kwa mwaka katika ngazi ya kaya.
- Kutoa taarifa za maendeleo ya kilimo na hali ya chakula kila wakati ngazi ya Wilaya, Mkoa na Kitaifa
- Kuratibu na kufuatilia upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile makampuni ya pembejeo, mawakala na wasambazaji wa pembejeo.
- Kuratibu na kufuatilia upatikanaji na matumizi ya zana bora za kilimo kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kutunza na kuweka takwimu za hali ya zana katika halmashauri.
- Kukusanya takwimu za kilimo kwa kila mwezi na kuzifikisha kwa wadau mbali mbali ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za kitaifa kwa mtandao uliunganishwa ujulikanao kama ‘Agricultural Routine Data System’ (ARDS).

- Kukusanya takwimu za upatikanaji na bei za mazao ya chakula na biashara katika masoko kila wiki na kila mwezi.
- Kuibua miradi kwa kufuata mbinu shirikishi jamii ya fursa na vikwazo katika maendeleo kuanzia ngazi ya vijihi na kuwezesha utekelezaji wa miradi hiyo chini ya Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Wilayani (DADPs)
- Kusimamia, kufuutilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Miradi ya Maendeleo ya Kilimo chini ya Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Wilayani (DADPs).
- Kwa kushirikiana na vituo vya utafiti vya Uyole idara huendesha mashamba ya majaribio ya uzalishaji wa aina mbali mbali za mazao.
- Kuanzisha, kusimamia na kuendesha vituo vya mafunzo ya wakulima na wafugaji vya kata (Ward Agricultural Resource Centers).
- Kuhamasisha uanzishaji wa vikundi vya wakulima.
- Kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika, kusimamamia uendeshaji wa vyama vya ushirika, kufanya ukaguzi wa vyama vya ushirika na kutoa taarifa katika vyama, kusimamia mikutano mikuu ya vyama vya ushirika na kusaidia kutatua migogoro ya vyama vya ushirika kwa kuzingatia kanuni na sheria ya vyama vya ushirika.

5.2 Njia zinazotumiwa kutoa huduma

Idara hutumia njia mbali mbali katika kufikisha huduma za ugani kwa wananchi. Njia hizo ni zifuatazo:

- Mafunzo kwa njia ya kutembelea wakulima mashambani
- Mafunzo kupitia vikundi na kuongea na vikundi
- Mafunzo kwa njia ya mabango na vipeperushi.
- Mafunzo kwa njia ya warsha na semina
- Mafunzo kwa njia ya mashamba ya mfano
- Mafunzo kwa njia ya mashamba darasa.
- Ziara za mafunzo nje na ndani ya wilaya
- Mafunzo kupitia maonesho mbalimbali kama vile maeneosho ya nane nane, siku ya wakulima n.k.
- Mafunzo kupitia vituo vya rasilimali za kilimo na mifugo vya kata (Ward Agricultural Resource Centre).

6.0 MWENENDO WA MVUA KWA MSIMU 2015/2016 NA 2016/2017

Mwenendo wa unyeshaji wa mvua katika wilaya kwa misimu miwili ya 2015/2016 na 2016/2017 ulikuwa wa kuridhisha kama inavyoainishwa katika jedwali na. 1 hapo chini. Wakulima wanaendelea na shughuli za kilimo kama kawaida.

Jedwali Na.1: Mwenendo wa mvua msimu 2015/2016 na 2016/2017

Mwenendo wa mvua Msimu wa Kilimo 2015/2016					
Na	Mwezi	Kituo cha Bomani		Kituo cha Lupatingatinga	
		Idadi ya siku	Kiasi cha mvua (mm)	Idadi ya siku	Kiasi cha mvua (mm)
1	Oktoba, 2015	-	-	3	5.6
2	Novemba, 2015	8	106.2	12	130.1
3	Desemba, 2015	12	211.4	18	174.1
4	Januari, 2016	17	356.4	28	304.3
5	Februari, 2016	9	145.3	20	154.8
6	Machi, 2016	7	146.7	17	158.9
7	April, 2016	4	68.9	9	157.2
8	Mei, 2016	-	-	1	0.1
	JUMLA	57.0	1,034.9	107	1,085.1

Mwenendo wa mvua Msimu wa Kilimo 2016/2017						
Na	Mwezi	Kituo cha Bomani		Kituo cha Lupatingatinga		Kituo cha Sangambi
		Idadi ya siku	Kiasi (mm)	Idadi ya siku	Kiasi (mm)	Idadi ya siku
1	Oktoba, 2016	0	0	0	0	0
2	Novemba, 2016	1	30.85	6	33.4	2
3	Desemba, 2016	11	170.38	21	158.5	11
4	Januari, 2017	13	125.77	21	146.5	10
5	Februari, 2017	8	199.16	11	77.4	10
6	Machi, 2017	11	232.9	12	153.7	17
7	April, 2017	14	139.13	14	143.5	11
8	Mei, 2017	6	43.17	3	42.19	5
	JUMLA	64	941.36	88	755.19	66
						660.98

7.0 UZALISHAJI WA MAZAO YA CHAKULA NA BIASHARA 2015/16 – 2016/17

Uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara umekuwa ukiongezeka kutoka mwaka hadi mwaka kutokana na kuiongezeka kwa maeneo yanayolimwa na kuiongezeka kwa wakulima wanaotumia mbegu bora, mbolea na zana bora za kilimo. Hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa miaka 2 ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.2 hapo chini.

Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa mazao kwa miaka 2 mfululizo (2015/2016 - 2016/2017)

Mazao	2015/2016		2016/2017	
	Eneo (Ha)	Mavuno (T)	Eneo (Ha)	Mavuno (T)
Mazao ya Chakula				
Mahindi	40,325	95,062	41,271	114,125
Mtama	2,589	2,914	1,995	3,319
Ulezi	1,453	793	581	534
Mpunga	1,268	1,804	710	2,441
Muhogo	590	1,517	325	1,549
Viazi vitamu	3,946	10,457	2,750	15,000
Kunde	1,012	598	598	424
Maharage	9,928	6,771	9,265	7,075
Jumla	61,111	119,915	57,495	144,468
Mazao ya Biashara				
Tumbaku	7,834	10,417	8,491	12,086
Alizeti	5,528	6,680	3,534	3,860
Ufuta	1,815	827	1,132	894
Karanga	7,519	5,897	5,507	5,586
Choroko	592	353	363	256
Jumla	23,295	24,174	19,027	22,683

8.0 MAFANIKIO

8.1 Hali ya Chakula

Wilaya imeendelea kujitosheleza kwa chakula katika kipindi cha 2015/2016 na 2016/2017. Pia matokeo ya tathmini ya awali ya mavuno katika msimu 2016/2017 yanaonyesha kuwa wilaya itajitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada katika kipindi cha 2017/2018.

Mahitaji ya chakula katika wilaya kuanzia kipindi cha 2015/2016 hadi 2017/2018 ni kama ilivyoainishwa hapo chini:-

Jedwali Na.3: Hali ya chakula kuanzia kipindi cha 2015/2016 hadi 2017/2018

Msimu	Mavuno yaliyopatikana (Tani)	Mahitaji ya Chakula		Ziada (Tani)
		Kipindi	Tani	
2014/2015	165,349	2015/2016	99,706	65,643
2015/2016	119,915	2016/2017	55,329	64,586
2016/2017	144,468	2017/2018	56,214	88,254

Wakulima kwa mara kwa mara hushauriwa kuhifadhi na kutunza vizuri mavuno yanayopatikana yenyе kutosheleza mahitaji ya chakula kwa mwaka mzima na kuепuka kuuza mazao ya chakula kutokana na vishawishi vya bei vinavyokuwepo wakati wa mavuno

8.2 Kuongeza uchumi na huduma za jamii kwa wananchi

Mazao ya biashara na sehemu ya mazao ya chakula yamekuwa yakichangia katika kuinua uchumi wa wananchi na mapato ya ndani ya Hamashauri kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali.

Katika kipindi cha 2015/16 na 2016/17, mchango wa Sekta ya Kilimo katika mapato ya ndani ya Halmashauri ulikuwa asilimia 54.02 kwa mwaka 2015/16 na asilimia 75.02 kwa mwaka 2016/17. Viwango hivi vya mchango ni kwa mujibu wa malengo ya Mpango na bajeti yaliyowekwa katika miaka husika. Jedwali Na. 4 linaonesha mchanganuo wa viwango hivyo.

Jedwali Na.4: Mchango wa Sekta ya Kilimo katika Mapato ya ndani ya Halmashauri kwa mwaka 2015/2016 na 2016/2017.

Mwaka	Vyanzo			Jumla	% ya machango wa kilimo
	Tumbaku	Mazao Mchanganiko	Vyanzo vingine		
2015/2016	2,064,685,300	450,000,000	2,140,186,528	4,654,871,828	54.02
2016/2017	1,786,423,750	162,000,000	631,486,250	2,579,910,000	75.52

8.3 Kuboresha thamani ya mazao

Halmashauri imejitahidi kuboresha myororo wa thamani wa mazao ya chakula na biashara.

Kwa upande wa mazao ya chakula, sekta binafsi imeendelea kuhamasishwa kuwekeza zaidi katika miundombinu mashine za kusindika mazao hasa mashine za kusindika nafaka. Mwitikio ni wa kuridhisha.

Pia katika mazao ya bishara, Halmashauri kwa kushirikina na sekta binafsi, vikundi vya wakulima na wabia wengine wa maendeleo, kumekuwa na uwekezaji katika kujenga jumla ya vituo 13 vya kusindika mafuta ya alizeti.

9.0 UPATIKANAJI WA PEMBEJEZO ZA KILIMO MSIMU 2015/2016 – 2016/2017

Pembejezo ni muhimu katika kufanya kilimo kuwa na tija. Pembejezo hizo ni mbolea za kupandia na kukuzia, madawa na mbegu bora ambazo hupatikana kuitia mfumo wa pembejezo za ruzuku zinazotolewa na Serikali na kuitia mawakala binafsi.

9.1 Pembejezo zenye ruzuku msimu 2015/2016 – 2016/2017

Serikali hutoa pembejezo za ruzuku kwa wakulima kwa kila msimu wa kilimo. Hata hivyo pembejezo za kilimo za ruzuku tunazopokea kutoka Serikalini zimekuwa zikipungua kutoka msimu hadi msimu, Hali hii imepelekea wakulima wengi wasio na uwezo wa kumudu kununua pembejezo kuzikosa na hatimaye tija kushuka.

Upatikanaji wa pembejezo za kilimo za ruzuku katika wilaya kuanzia msimu 2015/2016 hadi 2016/2017 ni kama ifuatavyo; -

Jedwali Na.5: Upatikanaji na matumizi ya pemebejezo za kilimo za ruzuku 2015/16 - 2016/17

Msimu 2015/2016 (Wanufaika 8,499)						
Na	Aina ya pembejezo	Mgawo	Pokelewa	Tumika	Baki	% ya utekelezaji
1	Mbegu ya mahindi (Kilo)	82,380	82,380	72,620	9,760	88.2
2	Mbolea ya kupandia (Mifuko)	8,592	8,592	8,502	90	99.0
3	Mbolea ya kukuzia (Mifuko)	8,499	8,499	8,489	10	99.9
Msimu 2016/2017 (Wanufaika 5,240)						
Na	Aina ya pembejezo	Mgawo	Pokelewa	Tumika	Baki	% ya utekelezaji
1	Mbegu ya mahindi (Kilo)	52,400	7,040	7,040	0	13
2	Mbolea ya kupandia (Mifuko)	5,240	2,709	2,709	0	52
3	Mbolea ya kukuzia (Mifuko)	5,240	5,050	5,050	0	96

9.2 Pembejezo zisizo za ruzuku

Katika msimu wa kilimo 2015/2016 na 2016/2017 wakulima walipata pembejezo zisizo na ruzuku kutoka vyanzo vingine vya pembejezo ambavyo ni vyama vya mazo hasa tumbaku na wafanya biashara binafsi.

Jumla ya Vyama 17 vya msingi vya wakulima wa tumbaku huwezeshwa mikopo ya pembejezo kuitia benki za NMB na CRDB. Kiasi cha pembejezo zilizopatikana kuitia utaratibu huu kwa misumu 2 ni kama ilivyoinishwa kwenye jedwali Na.6 hapa chini.

Jedwali Na.6: Mapokezi na matumizi ya pembejeo katika vyama vya msingi vya wakulima wa zao la tumbaku kwa mwaka 2015/2016 na 2016/2017.

Msimu 2015/2016 (Wanufaika 5,240)					
Na	Aina ya pembejeo	Pokelewa	Tumika	Baki	% ya utekelezaji
1	Mbegu ya mahindi (Kilo)	70,000	70,000	-	100
2	NPK 10:18:24 (Mifuko)	80,080	80,080	-	100
3	CAN 27%N (Mifuko)	20,960	20,960	-	100
4	UREA46%N (Mifuko)	19,200	19,200	-	100

Msimu 2016/2017 (Wanufaika 5,240)					
Na	Aina ya pembejeo	Pokelewa	Tumika	Baki	% ya utekelezaji
1	Mbegu ya mahindi (Kilo)	27,000	27,000	-	100
2	NPK 10:18:24 (Mifuko)	85,360	85,360	-	100
3	CAN 27%N (Mifuko)	23,060	23,060	-	100
4	UREA46%N (Mifuko)	22,020	22,020	-	100

Katika msimu wa kilimo 2016/2017 Halmashauri ilinunua kilo 1,942 za mbegu bora ya mtama aina ya macia zenyet thamani ya Tsh. 8,500,000/= na kuzifikisha kwa wakulima katika vijiji 23. Lengo lilikuwa ni kuwawezesha wakulima kupunguza athari za mtawanyiko wa mvua uliokuwa siowakuridhisha.

Pia katika msimu 2016/2017, Halmashauri ilinunua kilo 182 za mbegu bora ya ufuta aina ya Lindi 02 na kugawa kwa wakulima katika vijiji 10. Lengo ni kuongeza wigo wa mazao ya biashara.

10.0 MATUMIZI YA ZANA ZA KILIMO

Katika kutekeleza shughuli za Kilimo wakulima wa Wilaya wa chunya wanalazimika kutumia zana za Kilimo na nyenzo mbalimbali ili kufikia malengo yao

Taarifa ya zana za kilimo zitumikazo wilayani chunya ni kama inavyooneshwa kwenye jedwali na 4 hapo chini:-

Jedwali Na. 5: Zana za Kilimo

Na.	Aina ya zana za Kilimo	Idadi ya zana
1	Matrekta makubwa	39
2	Matrekta madogo (powertillers)	36
3	Majembe ya kukokotwa na wanyama	3,684
4	Majembe ya Mkono	145,849
	JUMLA	149,608

Hata hivyo upatikanaji na matumizi ya zana bora za kilimo kwa wakulima bado yako chini ikilinganishwa na idadi ya kaya za wakulima na zana za kilimo zilizopo katika wilaya.

Ili kuongeza matumizi zaidi ya zana bora za kilimo, wilaya inaendelea kuhamasisha wakulima kununua na kutumia ya zana bora za kilimo.

11.0 SEKTA YA UHIRIKA

MCHEPUO	IDADI	MADHUMINI	NAFASI YA HALMASHAURI	MAFANIKIO
MAZAO	Zao la Tumbaku 19.	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Kupata masoko ya mazao (tumbaku), ➤ Kupata mokopo kwa ajili ya mitaji ya kuendesha biashara ya kilimo, ➤ Kupata pembejeo na zana za kilimo kwa urahisi, 	<p>Kuwezesha Ofisi ya kilimo, umwagiliaji na Ushirika ili kuweza;</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Kusimamia zao la tumbaku kwa kushirikiana na wadau, ➤ Kufanya Ukaguzi wa shughuli za vyama vya Ushirika, ➤ Kuviwezesha vyama kupata Mikopo ya kilimo ambayo inawasaidia kupata mitaji ya kuendeshea Kilimo cha tumbaku. 	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Wakulima wanapata pembejeo za kilimo cha zao la tumbaku kwa wakati, ➤ Wakulima wanalipwa malipo yao ya mauzo ya tumbaku kwa wakati, ➤ Mikopo inayokopwa na Vyama inalipwa kwa wakati na kwa asilimi 100, ➤ Uwepo wa Vyama imara na vyenye maendeleo yanayoonekana. ➤ Zaidi ya watu 7,000 wameajiliwa katika tasnia hii ya tumbaku. ➤ Chanzo kukibwa cha Mapato ya Halmashauri ni Ushuru wa Tumbaku. ➤ Mahusiano ya Halmashauri na Wadau wengine katika tasnia ya tumbaku ni mazuri na Imara.
	Mazao Mchanganyi 5.	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Kupata masoko ya mazao mchanganyiko (Alizeti, Mahindi, n.k) ➤ Kuongeza thamani ya mazao kwa njia ya usindikaji wa mazao, ➤ Kupata pembejeo na zana za kilimo kwa urahisi, ➤ Kujenga nguvu ya masoko ya mazao ya Wanachama, 	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Kuviwezesha Vyama kupata Mashine ndogo kwa ajili ya usindikaji wa Alizeti, ➤ Kupanga mikakati ya kuwezesha Mfumo wa stakabadhi ghalani, ➤ Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa shughuli za vyama kwa kuzingatia sheria ya Ushirika. 	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Vyama vya Umako, Matundas, Mtakaiga na Muungano vinamashine ndogo za kukamulia mafuta ya alizeti.
AKIBA NA MIKOPO	SACCOS 11	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Kutoa hudhuma za kifedha kwa masharti nafuu kwa Wanachama, 	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa shughuli za vyama kwa kuzingatia 	<ul style="list-style-type: none"> ➤ SACCOS 8 ziko hai na zinatoa huduma za mikopo kwa Wanachama,

		<ul style="list-style-type: none"> ➤ Kupata Elimu ya Biashara na Ujasiliamali, ➤ Kukuza mitaji ya Biashara za Wanachama 	<ul style="list-style-type: none"> ➤ sheria ya Ushirika. ➤ Kutoa Elimu ya Biashara na ujasiliamali kwa Wanachama wa SACCOS. 	
MIFUGO	MIFUGO 3	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Kupata Masoko ya mazao ya mifugo, ➤ Kuwezesha Huduma za Ugani na; ➤ Kupata nguvu ya kutatua changamoto za Ufugaji kwa Wanachama. 	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Kutoa huduma za Ugani kwa Wanachama, ➤ Kuwezesha vyama kupata miundombinu wezeshi kwa ajili ya ufugaji bora wa mifugo. ➤ Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa shughuli za vyama kwa kuzingatia sheria ya Ushirika. 	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Vyama 2 ni hai na vinafanya kazi iliyokusudiwa. ➤ Chama cha Hiariyamoyo, kinakusudia kujenga miundombinu ya Mifugo ikiwa ni pamoja na Josho (litagharimu kiasi kisichopungua 10,000,000/= mwaka, 2017). Mipango ya baadaye ni kujenga Rambo na kuwa na Duka la madawa la chama.
UVUVI	UVUVI 1	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Kuendesha uvivu wa kisasa na wenyе tija baina ya Wanachama, ➤ Kupata Masoko ya samaki na mazao ya Samaki, ➤ Kuwawezesha Wanachama kupata mitaji ya kuendeshea biashara ya samaki. 	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Kutoa huduma za Ugani kwa Wanachama, ➤ Kuwezesha vyama kupata miundombinu wezeshi kwa ajili ya ufugaji bora wa Mifugo. ➤ Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa shughuli za vyama kwa kuzingatia sheria ya Ushirika. 	<ul style="list-style-type: none"> ➤ Chama cha UWASA FCS cha Makongolosi, kimejenga mabwawa mawili ya samaki yaliyogharimu jumla ya sh. 10,000,000/=, ➤ Wanachama wamewezechwa Mikopo toka Mfuko wa chama jumla sh. 5,000,000=.

12.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO (ASDP/DADPS) KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016 NA 2016/2017

Miradi mbalimbali inaendelea kutekelezwa kwa kutegemea mapato ya ndani. Ktika kipindi tajwa, jumla ya **Tsh 75,730,000/=** zimetumia kutekeleza miradi na shughili mbalimbali kama ifuatavyo:

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2015/2016

SHUGHULI ILIYOFANYIKA	KIASI (TZS)	CHANZO	MATOKEO (TIJA)	MATARAJIO
Kuimarisha uzalishaji wa zao la mpunga kwa njia ya mashamba darasa - Skimu Ifumbo	17,700,000	MAPATO YA NDANI - MAENDELEO	Wakulima 18 na maafisa kilimo 2 walipata mafunzo ya kilimo bora cha mpunga ngazi I na ya II MATI - Igurusu na Skimu Ifumbo ambapo wakati wa mavuno tija iliyofikiwa ni 6t/ha.	Wakulima wengi wameongeza maeneo ya kilimo cha mpunga
Kumalizia ujenzi wa vituo vya usindikaji wa alizeti katika vituo vya Ifumbo na Mamba	10,000,000	MAPATO YA NDANI - MAENDELEO	Umaliziaji wa majengo ya vituo vya kusindika alizeti kwa ajili ya kuongeza thamani ya zao la alizeti katika kata ya Ifumbo na Mamba umekamilika, usindikaji unaendelea.	Thamani ya mafuta ya imeongezeka, kipato ngazi ya kaya kimeboreshwa
Kuwezesha usambazaji na usimamizi wa pembejeo za ruzuku katika Tarafa za Kiwanja na Kipembawe.	7,900,000	MAPATO YA NDANI - MAENDELEO	Usimamizi wa matumizi ya pembejeo za ruzuku umefanyika. Jumla ya kilo 80,103 za mbegu bora ya mahindi, mifuko 9,491 ya mbolea ya kupandia na mifuko 9,789 ya mbolea ya kukuzia zimetumika. Asilimia ya jumla ya utekelezaji ni 88.	Uzalishaji wa mazao umeongezeka, wilaya kujitosheleza kwa chakula
Kuwezesha upatikanaji wa tani 2 za mbegu za dharura za mtama katika Tarafa ya Kiwanja	3,500,000	MAPATO YA NDANI - MAENDELEO	Tani 3.5 za mbegu ya mtama zililetwa na kusambazwa kwa wakulima msimu 2013/14	Wilaya kujitosheleza kwa chakula
JUMLA	39,100,000			

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2016/2017

SHUGHULI ILIYOFANYIKA	KIASI (TZS)	CHANZO	MATOKEO (TIJA)	MATARAJIO
Kuimairisha Vyama vya ushirika vya msingi 5 vya mazao ya ufuta na alizeti katika vijiji vya Sangambi, Mtanila, Makongolosi, Matundasi na Chalangwa	1,250,000	MAPATO YA NDANI - MAENDELEO	Wanachama wa vyama vya ushirika vya msingi 5 na vikundi vya wakulima 2 wamepata mafunzo ya ujasiriamali, taratibu za fedha na utunzaji wa kumbukumbu.	Kuinua kipato kwa wakulima kwa kuimarisha vyama vya ushirika vya mazao ya ufuta na alizeti
Kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora ya Ufuta na Mtama	5,250,000	MAPATO YA NDANI - MAENDELEO	Jumla ya kilo 182 za mbegu ya ufuta na kilo 942 za mtama zilinunuliwa na kufikishwa kwa wakulima bure	Kuongeza wigo na tija ya mazao ya chakula na biashara kwa wakulima
Ufuatiliaji wa usambazaji na matumizi ya pembejeo za kilimo za ruzuku msimu 2016-17	2,100,000	MAPATO YA NDANI - MAENDELEO	Ufuatiliaji wa usambazaji na matumizi ya pembejeo za ruzuku umefanyika katika vijiji 43. Jumla ya mifuko 2,610 ya mbolea ya kupandia, mifuko 5,240 ya mbolea ya kukuzia na kilo 5,400 kgs za mbegu ya mahindi zimefikishwa kwa wakulima.	Kuongeza wigo na tija ya kwa mazao ya chakula na biashara kwa kufikisha pembejeo bora kwa wakulima
Kuwezesha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za kilimo mfumo wa ARDS	17,300,000	MAPATO YA NDANI - MAENDELEO	Pikipiki 5 , madaftari ya ugani 40 na vitabu vya kutunzia kumbu kumbu (Diary) 40 kwa ajili maafisa ugani vimenunuliwa na kusambazwa kwa maafisa ugani.	Uboreshaji wa utoaji wa huduma za ugani
Kuwezesha uzalishaji wa mbegu bora daraja la kuazimiwa kwa mazao ya alizeti na ufuta	4,910,000	MAPATO YA NDANI - MAENDELEO	Mbegu bora ya alizeti tani 1.5 imezalishwa katika kata ya makongolosi kwa ushirikiano kati ya Halmashauri na MWAMKO AMCOS Makongolosi	Mbegu bora ya alizeti kupatikana kwa wakulima msimu 2017/18
Kukamilisha ujenzi wa vituo 2 vya kusindika alizeti katika vijiji vya Ifumbo na Mamba	5,820,000	MAPATO YA NDANI - MAENDELEO	Umaliziaji wa majengo ya vituo vya kusindika alizeti kwa ajili ya kuongeza thamani ya zao la alizeti katika kata ya Ifumbo na Mamba umekamilika, usindikaji unaendelea.	Thamani ya mafuta ya imeongezeka, kipato ngazi ya kaya kimeboreshwa
JUMLA	36,630,000			

13.0 CHANGAMOTO

- (1) Tangu mwaka wa fedha 2015/2016 Halmashauri haijapokea fedha kutoka serikali kuu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya kilimo
- (2) Pembejeo za kilimo za ruzuku hutolewa kiasi kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya wakulima. Hivyo wakulima wenye uwezo mdogo hushindwa kumudu kununua pembejeo kwa bei ya soko.
- (3) Bajeti inayotolewa kwa ajili ya matumizi mengine ni ndogo kwa ajili ya kilimo. Hata hicho kiasi kidogo hakitolewi.
- (4) Upungufu wa watumishi kulingana na mahitaji. Mahitaji ni watumishi 70 wa kada mbali mbali lakini waliopo ni watumishi 33 tu.

14.0 MIKAKATI

14.1 Mikakati ya kukabiliana na uhaba wa chakula

- 1) Wananchi wameshauriwa kutumia vizuri chakula kilichopo, ikiwa ni pamoja na kupunguza matumizi ya nafaka kupikia pombe.
- 2) Wananchi wamehamashishwa kutochagua chakula
- 3) Wafanya biashara wasiendelee kuuza chakula nje ya Wilaya.
- 4) Wakulima na wafugaji wameelekezwa kuuza mazao ya biashara kupata fedha badala ya kuuza mazao ya chakula.
- 5) Wakulima wamehamasishwa kulima mazao yanayokomaa haraka na yanayostahimili ukame.

14.2 Mikakati ya kuongeza eneo la kilimo na tija

- 1) Kutoa elimu kwa wakulima kwa kuititia mfumo wa mashamba darasa kwa kila kata.
- 2) Kuwashauri wakulima kutumia kikamilifu wanyama kazi waliopo.
- 3) Kuhimiza matumizi ya mbolea ya asili (samadi), mbolea ya viwandani na mbegu bora.
- 4) Kuhakikisha matrekta yanatumika kikamilifu. Hadi sasa katika Wilaya kuna matrekta madogo 36 na matrekta makubwa 39.
- 5) Kuendelea kuboresha skimu za umwagiliaji.

- 6) Kuhimiza wananchi kukopa matrekta na kukarabati yale yaliyoharibika.
- 7) Kuajiri maafisa ugani 23 wa kata na vijiji.
- 8) Kuhamasisha uanzishaji wa stakabadhi ya mazao ghalani

14.3 Mikakati ya Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Wilayani (DADPs)

- 1) Kuibua miradi kwa kufuata mbinu shirikishi ya fursa na vikwazo katika maendeleo kuanzia ngazi ya vijiji na kuwezesha miradi inayopelekea kuongezeka kwa tija na faida katika kumudu nguvu ya soko.
- 2) Kuendeleza zao la kipaumbele kwa kuzingatia mnyororo wa thamani ambapo kwa wilaya ya chunya zao la kipaumbele ni alizeti.
- 3) Kuimarisha huduma za ugani ikiwa ni pamoja na kujenga na kutumia vya Raslimali za Kilimo vya Kata (Ward Agricultural Resource Centers)
- 4) Kuimarisha umoja na vyama vya wakulima
- 5) Kuendeleza skimu ya umwagiliaji ya kijiji cha Ifumbo.

15.0 WATUMISHI

Hali ya watumishi katika idara ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwali lifuatalo:

MAHALI	KADA	MAHITAJI	WALIOPO		UPUNGUFU
			Wanaume	Wanawake	
Makao Makuu ya Halmashauri	Afisa Kilimo	7	5	0	2
	Mhandisi wa Umwagiliaji	1	0	0	1
	Afisa Matumizi Bora ya Ardhi	2	0	0	2
	Mpimaji (Surveyor)	2	0	0	2
	Fundi Sanifu wa Umwagiliaji na Ujenzi	2	0	0	2
	Mhandisi wa Kilimo	1	0	0	1
	Fundi Sanifu wa Zana za Kilimo	1	0	0	1
	Afisa Ushirika	5	2	0	3
Jumla Ndogo		21	7	0	14
Vijiji na Kata	Afisa Kilimo Msaidizi	49	19	7	23
	Jumla Ndogo	49	19	7	23
	JUMLA KUU	70	26	7	37

16.0 MUUNDO WA IDARA

Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika ina vitengo vitano. Vitengo hivyo ni Huduma za ugani, Takwimu, Mazao, Umwagiliaji na Ushirika. Muundo wa Idara ni kama inavyoonekana kwenye mchoro ufuatao:

